

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS-TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA TUNDURU**

**TANGAZO LA ZABUNI**



22 / 01 / 2018

**UJENZI NA UKAMILISHAJI WA KITUO CHA AFYA MKASALE**

**Zabuni Na. LGA/106/2017/2018/W/MKASALE/01**

1. Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru imepokea fedha kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya ujenzi na ukamilishaji wa kituo cha Afya Mkasale.
2. Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru anakaribisha maombi kutoka kwa mafundi wenye sifa na uzoefu katika fani ya ujenzi kwa ajili ya ujenzi na ukamilishaji wa kituo cha Afya Mkasale.
3. Tangazo hili linapatikana kwenye mbao zote za matangazo kituo cha afya Mkasale, na mbao zote za matangazo za Halmashauri ya Wilaya Tunduru.
4. Mafundi walio sifa na uwezo wanaweza kupata taarifa kuhusu taarifa hizi kwenye ofisi ya Katibu wa Bodi ya Zabuni, Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru S.L.P 275, Tunduru. Ofisi Na. 35 au 36 kuanzia saa 3.00 asubuhi hadi saa 9.00 alasiri, Jumatatu hadi Ijumaa isipokuwa siku za sikukuu.
5. Nyaraka nyingine zinazohusiana na tangazo hili ( michorona mchanganuo wa kazi zitakazofanyika) zinapatikana ofisi ya Katibu wa Bodi ya Zabuni kwa fundi kuwasilisha maombi yake kimaandishi kwa Mkurugenzi Mtendaji, Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru S.L.P 275, Tunduru.

6. Baada ya fundi kupata mchanganuo wa kazi za kufanya atatakiwa kuwasilisha gharama za ujenzi wa kituo cha afya Mkasale. Halmashauri kwa kushirikiana na kamati ya ujenzi itanunua vifaa/bidhaa na fundi atakuwa na jukumu la kufanya ujenzi na kazi nyingine zitakazoainishwa na msimamizi wa ujenzi.
7. Majengo yanayotarajiwa kujengwa ni kama ifuatavyo:-
  - a) Jengo la Upasuaji (Theatre)
  - b) Wodi ya kina mama (Female ward)
  - c) Wodi ya watoto (Children's ward)
  - d) Maabara (Laboratory)
  - e) Nyumba ya mtumishi inayojitegemea (Staff house)
  - f) Chumba cha kuhifadhia maiti (Mortuary)
  - g) Kichomea taka (Incinerator) na shimo la kutupia kondo la nyuma (Placenta pit)
8. Sifa za mwombaji ( Local Fundi's)
  - a) Mwombaji awasilishe vielelezo vya kuonyesha sifa , uwezo na uzoefu wa kujenga majengo ya serikali.
  - b) Awe na uwezo wa kutafsiri michoro(drawings) pamoja na maelezo mengine ya kitaalam (specifications).
  - c) Awe na uwezo wa kufanya kazi kwa kuzingatia kanuni na taratibu za Serikali (Mzalendo na mwaminifu)
  - d) Awe Mtanzania Mwenye umri usiopungua miaka 18
9. Maombi yote yawasilishwe kwenye nakala halisi moja na nakala mbili (2) kivuli (copy) yakiwa yamefungwa vizuri kwenda kwa Katibu wa Bodi ya Zabuni, Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru S.L.P 275, Tunduru, kabla au siku ya tarehe 01/02/2018 saa 8.00 mchana, ikifuatiwa na ufunguzi wa zabuni hizo mbele ya waombaji au wawakilishi wao. Juu ya bahasha yaandikwe maneno, MAOMBI YA ZABUNI YA UJENZI NA UKAMILISHAJI WA KITUO CHA AFYA MKASALE
10. Zabuni itakayoletwa kwa kuchelewa au ikiwa haijafungwa haitapokelewa kwa ajili ya ufunguzi.



MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
TUNDURU

MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA  
TUNDURU